

# Utafiti: Mto Msimbazi chanzo mbu Muhimbili

Na Marlana Mathias

BONDE la Mto Msimbazi jijini Dar es Salaam limekuwa tishio kwa kuzalisha mbu na kusababisha milipuko ya magonjwa ya malaria kuongezeka kwa kasi katika maeneo yaliyopita mto huo hasa Hospitali ya Muhimbili.

Hayo yalibainishwa juzi na mtafiti kutoka taasisi ya utafiti wa masuala ya kijamii na kiuchumi

(ESRF), Francis Mwaijande, katika mkutano wa kujadili taarifa ya utafiti wa ongezeko la mbu alioufanya katika Bonde la Mto Msimbazi Julai, mwezi 2010.

Alisema katika utafiti huo asilimia 91 ya wafuatilaji taarifa hiyo walikubali kuwa mto huo unasababisha mazalia ya mbu kwa kiasi kikubwa na kusababisha mbu kujaa katika maeneo hayo hasa Hospitali ya Muhimbili na hivyo

vifo kuongezeka.

Mto huo umekuwa ukikusanya majitaka kutoka maeneo mbalimbali ya makazi ya watu na viwanda na kuwa tishio kwa kuzalisha mbu na kusababisha vifo vingi vitokanavyo na ugonjwa wa malaria.

Mwaijande alisema kuwa miundombinu mibovu na kujenga viwanda katika maeneo ya watu bila kuwepo uhabibi wa utiririshaji

maji imepelekea majitaka kutuama hovy katika maeneo hayo.

Aliongeza kuwa mazingira mengi yakiwemo mapori yamekuwa yakizalisha na kuhifadhi mbu hasa katika kipindi cha mvua kwa sababu ya kutosafishwa.

Pia washiriki wa utafiti huo walisema uwajibikaji wa viongozi umekuwa finyu na kutoa mfano

halisi wa wilaya ya Moshi wanavyodhibiti usafi wa mazingira kwa sababu ya uongozi mzuri uliopo.

Aidha, wameitaka serikali itenge bajeti kwa ajili ya kukabiliana na ugonjwa wa malaria na pia wamependekeza siku ya usafi itengwe na iwe rasmi kwa kila mwananchi kuhusika na usafi wa mazingira anayoishi na viongozi wapite kugagua maeneo yote.